

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA

### MUHTASARI WA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KWA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 26/03/2018

#### Mhe. Mwenyekiti;

Rasimu ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 imeandaliwa katika sehemu kuu tatu (3) nazo ni: -

1. Mapitio ya Bajeti ya Mwaka 2016/2017
2. Mapitio ya Bajeti ya Nusu mwaka 2017/2018
3. Rasimu ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019

#### 1.0 MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/2017

#### Mhe. Mwenyekiti;

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Kondoza iliidhinishwa kutumia jumla ya **Tsh. 31,693,623,570.00**. Hadi kufikia Juni 30, 2017 Halmashauri ilikuwa imekusanya jumla ya **Tsh. 26,478,453,467.00** sawa na **83%** ya Bajeti idhinishwa na kufanya jumla ya fedha iliyokuwepo kuwa **Tsh. 29,150,247,213.00** (pamoja na salio anzia **Tsh. 2,671,793,746.00**) na jumla ya **Tsh. 27,214,392,720.00** zilitumika sawa na **86%** ya Bajeti idhinishwa na sawa **93%** ya fedha zilizokuwepo.

Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jedwali hapo chini: -

S/n	Maelezo	Kiasi (Tsh.)				
		Idhinishwa	Pokelewa	%	Tumika	%
1	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)	1,219,777,892	443,754,010	36	443,754,010	100
2	Ruzuku ya Mishahara (PE)	20,579,135,800	18,135,558,444	88	18,207,182,690	100
3	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	8,700,939,394	6,807,710,175	78	7,772,403,233	114
4	Mapato ya Ndani	1,193,770,484	1,091,430,838	91	877,241,838	80
<b>Jumla</b>		<b>31,693,623,570</b>	<b>26,478,453,467</b>	<b>83</b>	<b>27,300,581,771</b>	<b>86</b>

**NB:** Fedha pokelewa ya mapato ya ndani inajumuisha fedha za CHF **Tsh. 214,189,000.00**

Shughuli/Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na: -

- Visima 28 vimechimbwa kwa jitihada za Mhe. Dr. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango (Mbunge wa Jimbo la Kondoza) ambapo visima virefu ni 21 na vifupi 6. Visima virefu vilivyochimbwa ni pamoja na Cheke, Dakula, Nanakwi, Isusumya, Pilili, Ikengwa, K/bwawani, K/majengo, K/kati, Salanka, Makafa/Kwadelo, Puh, mkekena, kwadinu, humai, bonga (chudi), bonga (ngwalaji), Ikova, mkundulu, thawi juu na Masawi

na Visima Vifupi ni pamoja na S/m Kalamba, Arya, Sangasanga, Makirya – Haubi, Bara, Mahindi, Swaga swaga.

- Matengenezo ya kiwango cha changarawe ya Barabara ya Gubali – Haubi – Ntomoko, Haubi – Pahi ambapo km 15 zimechongwa, kumwagwa kifusi na kushindiliwa pia kalavati 14 zimejengwa.
- Madawati mapya 755 ya sekondari na 2,090 ya shule za msingi yalitengenezwa na kusambazwa shuleni
- Vikundi 4 vya Vijana vilikopeshwa fedha kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi. Vikundi hivyo ni Rafiki Group, Hapa Kazi, Muungano na Sakatonge.
- Fimbo nyeupe 45 ziligawiwa kwa watu wasioona 45 waishio kandokando ya Barabara ya Arusha – Dodoma
- Ghala kubwa la kuhifadhi mazao lenye uwezo wa kuhifadhi tani 7,000 kwa wakati mmoja limejengwa katika Kijiji cha Pahi
- Wanavikundi 3,440 wamepata mafunzo juu ya Kilimo bora na upatikanaji wa masoko kupitia program ya MIVARF
- Madarasa 6 mapya yamejengwa, vyumba 3 vya madarasa vimekarabatiwa na choo cha matundu 10 kimejengwa shule ya msingi Kwadelo
- Mabweni 2 yenye uwezo wa kubeba Wanafunzi 64 kila moja yamejengwa Sekondari ya Masawi
- Madarasa 3 na choo matundu 10 vimejengwa na nyumba 1 ya Mwalimu imejengwa shule ya msingi Soro.
- Uhawilishaji fedha kwa Kaya 10,132 umeendelea kufanyika
- Zahanati ya Kwahengwa na Wodi katika Zahanati ya Pahi vimekamilika

## **2.0 MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA 2017/2018**

### **Mapato na Matumizi**

#### **Mhe. Mwenyekiti;**

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imeidhinishiwa kukusanya na kutumia **Tsh. 30,582,322,901.00**. Hadi kufikia Disemba 31, 2017 jumla ya **Tsh. 15,367,353,432.00** sawa na **50%** ya Bajeti iliyoidhinishwa zimepokelewa na kufanya jumla ya fedha zilizokuwepo kuwa **Tsh. 16,975,691,993 .00** (pamoja na fedha za salio anzia **Tsh. 1,608,338,560.00**) na **Tsh. 12,106,278,603 .00** sawa na **71%** zimetumika ya fedha zilizokuwepo.

Jedwali hapo chini linaonyesha mchanganuo wa Mapato na Matumizi:-

S/n	Maelezo	Kiasi (Tsh.)				
		Bajeti	Mapato		Matumizi	
			Kiasi	%	Kiasi	%
1	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)	2,032,805,196	1,445,828,433	71	676,153,032	47
2	Ruzuku ya Mishahara (PE)	17,195,082,200	8,096,562,073	47	8,069,834,100	100
3	Ruzuku ya Maendeleo (DEV)	9,669,396,505	5,467,435,026	56	3,124,710,052	57
4	<b>Mapato ya Ndani (OS)</b>	1,324,039,000	262,793,900	20	257,279,822	98
<b>Jumla Kuu</b>		<b>30,582,322,901</b>	<b>15,363,113,432</b>	<b>50</b>	<b>12,106,278,603</b>	<b>79</b>

### 2.1 Shughuli zilizotekelezwa/zinazoendelea kutekelezwa: -

- Ujenzi wa Kituo cha Afya Mauno unaendelee (Fedha zimepokelewa mwezi Oktoba 2017)
- Ukarabati mkubwa wa Kituo cha Afya Busi unatarajia kuanza mwezi Januari 2018 (Fedha zimepokelewa mwezi Januari 2018)
- Ukamilishaji wa ujenzi wa mabweni 2 yenye kulaza watoto 80 kila 1, madarasa 3 na choo cha matundu 6 katika Shule ya Sekondari Abed Aman Karume unaendelea. (Fedha zilipokelewa mwezi Mei 2017)
- Uboreshaji wa Miundombinu ya majengo katika Shule ya Msingi Kalamba na Soro umeanza Januari 2018
- Ujenzi wa shule za Sekondari 2 mpya katika Kata za Hondomairo na Bumbuta. (Fedha zimepokelewa mwezi Januari 2018)
- Ukarabati na ukamilishaji wa mabweni 2 katika Shule ya Sekondari Bereko umefanyika. (Kazi imefanyika kwa mapato ya ndani ya Kata ya Bereko)
- Visima virefu 13 vya maji vimechimbwa kati ya visima 27 Vilivyo kwenye mpango na kazi ya uchimbaji katika maeneo mengine 14 inaendelea. Kazi ya uchimbaji inafanywa na Wakala wa Uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa (DCCA)
- Ujenzi wa daraja la Kisese unaendelea
- Matengenezo makubwa ya Barabara ya Munguri – Thawi – Bereko yanaendelea

## **2.2 Changamoto**

Katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Kawaida na zile za Maendeleo kwa kipindi hiki cha kuanzia Julai hadi Disemba 2017, kumekuwa na changamoto zifuatazo: -

- Kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi mfano fedha za Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG), Ruzuku ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEDP) na Ruzuku ya UKIMWI (NMSF)
- Ushiriki hafifu wa Wananchi katika shughuli za maendeleo na kuendelea kutegemea Serikali katika kukamilisha miradi yao
- Uwepo wa Migogoro ya ardhi ambayo inazorotesha shughuli za maendeleo
- Upungufu wa watumishi kwa sekta zote
- Upungufu wa vitendea kazi (Upungufu wa magari)
- Vijiji vingi kukosa miundombinu ya Barabara na Umeme hali inayosababisha Wawekezaji kutovutiwa kuwekeza Kondo

## **2.3 Mikakati**

- Halmashauri kuiomba Serikali Kuu kuleta fedha kwa wakati
- Halmashauri inaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ili kupunguza utegemezi kwa Serikali.
- Kuendelea kupunguza matumizi katika shughuli za kawaida (recurrent activities) na kuelekeza fedha katika ya shughuli za msingi kwa kipaumbele
- Halmashauri inaendelea kufanya utatuzi wa migogoro ya ardhi iliyopo na kutoa Elimu kwa ajili ya kupunguzwa uzalishwaji wa migogoro na pia kutenga bajeti ya kutosha katika masuala ya ardhi kama kuandaa na kusimamia Mipango ya matumizi bora ya Ardhi
- Halmashauri imeomba vibali vya ajira utumishi wa umma
- Kuendelea kuiomba Serikali Kuu kusogeza huduma za umeme na Barabara kwenye maeneo yanayofaa kwa uwekezaji
- Halmashauri imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa magari yaliyopo wakati mikakati ya kutafuta fedha ya ununuzi wa magari mapya inaendelea kufanyika
- Kuendelea kuweka Mikakati ya kuongeza mapato ya ndani kwa kubuni vyanzo vipya na kuimarisha makusanyo
- Kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kupanga Ardhi, kupima na kurasimisha ili kuongeza uwekezaji

## **3.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019**

Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2018/2019 yanazingatia mambo muhimu yafuatayo: -

- Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)
- Dira ya Taifa ya Maendeleo (NDV) 2025
- Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) 2016/2017 – 2020/2021
- Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020

- Hotuba ya Rais ya Ufunguzi wa Bunge la 11
- Maamuzi ya Serikali ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma
- Sera mbalimbali za ki Sekta
- Miongozo kutoka Serikali Kuu
- Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti 2018/2019
- Maagizo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI wakati wa ufunguzi wa Kikao kazi cha kujadili Bajeti za LGDG 2017/2018

### 3.1 UMBILE NA MWELEKEO WA BAJETI MWAKA 2018/2019

Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya Kondoa imepanga kukusanya jumla ya **Tshs. 30,610,933,906.00** kwa mchanganuo ufuatao:

Ruzuku ya Matumizi Mengineyo	2,188,640,848.00
Ruzuku ya Mishahara	15,373,360,600.00
Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	12,482,479,362.00
Mapato ya Ndani	1,097,253,064.00

Mchanganuo wa Ruzuku za Miradi ya Maendeleo Tsh. **12,482,479,362.00** ni kama ifuatavyo: -

S/n	Jina la Program/Mradi	Makisio (Tsh.)
1	Mapato ya Ndani (Own Source)	529,800,000
2	Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG)	1,305,304,000
3	Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Vijijini (RWSSP)	5,062,999,968
4	Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF)	641,526,000
5	Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (LDF)	10,415,000
6	Program ya Kupambana na UKIMWI (TACAIDS)	16,000,000
7	Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)	51,657,000
8	TASAF III	4,467,808,356
9	EQUIP – Tanzania	396,969,038
<b>Jumla</b>		<b>12,482,479,362</b>

## 3.2 MAENEO YA KIPAUMBELE

Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2018/2019 yanazingatia kutekeleza maeneo yafuatayo ya kipaumbele: -

### 3.2.1 Kukuza Uchumi wa Ndani

#### 3.2.1.1 Viwanda na Biashara

- Kuwezesha Vijana kiuchumi kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya useremala katika Vijiji vilivyopo katika Barabara kuu ya Dodoma – Kondoa – Arusha.
- Kuwezesha uanzishaji wa kiwanda kidogo cha kusindika mazao ya Mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi katika Kijiji cha Bukulu Kata ya Soera. Kiwanda ambacho kitajengwa pembezoni mwa Barabara kuu ya Dodoma – Kondoa – Arusha.
- Kuwezesha Vijana kiuchumi kwa kuanzisha kiwanda kidogo cha ushonaji wa mavazi katika Kijiji cha Mnenia Kata ya Mnenia. Uwezeshaji huu utaenda sambasamba na uboreshaji wa Viwanda vidogo vya ushonaji nguo vilivyopo Thawi (Kikundi cha Moyowirude) na Chubi Kiwanda hiki kinatarajiwa kufanya kazi kwa kushirikiana na Kikundi cha uzalishaji wa batiki cha Mnenia (SAKATONGE).
- Kuanzisha Kiwanda cha usindikaji wa mafuta ya kula yatokanayo na mazao ya Alizeti na Ufuta katika Kijiji cha Pahi ambapo tayari ghala kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi tani 7,000 za alizeti limejengwa na kukamilika.
- Kuwezesha uwekezaji katika Kijiji cha Boma ya Ng'ombe kata ya Kwadelo ambapo tayari mwekezaji MANGALA FARM ameanza kuwekeza kwa kujenga majengo ya watumishi, kuchimba visima vya maji na kulima mazao eneo la ekari 500. Aidha anatarajia kuanza kujenga Kiwanda cha Maji, Kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti na ufuta na kiwanda cha kukoboa mpunga katika Kijiji cha Ihari na Kwadelo.
- Kufanya utafiti wa uanzishaji wa Viwanda vidogo vya utengenezaji wa vyombo vya udongo (Sahani, vikombe, bakuli, glasi, birika, n.k)
- Kuwezesha kikundi kimoja cha vijana kuanzisha kiwanda kidogo cha kusindika mazao ya nyuki (Asali, Nta, Gundi ya nyuki na Mbolea)
- Kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wafanya biashara wadogo na umuhimu wa kulipa tozo mbalimbali.

**NB: Ushawishi unaendelea kwa shirika la viwanda vidogovidogo SIDO - Dodoma kwa ajili ya kuja kuwekeza viwanda vidogovidogo kwa Vijana wa Kondoa**

### 3.2.1.2 Kilimo na Umwagiliaji

- Kuongeza thamani ya zao la Alizeti kwa kuvutia uwekezaji kwa kujenga **kiwanda cha ukubwa wa kati cha kuchakata mafuta ya alizeti** katika Kata ya Pahi ambapo tayari barabara ya Wilaya yenye urefu km 27 na barabara kuu ya Great North Road zinazounganisha Kata ya Pahi na Miji/Wilaya/Mikoa ya jirani zinaendelea kufanyiwa matengenezo makubwa, pia ghala kubwa la kuhifadhia mazao kiasi cha tani 7,000 kwa wakati mmoja katika Kata ya Pahi limekamilika.
- Kuongeza uzalishaji wa mazao ya mahindi kutoka tani 2 hadi 5 kwa hekta, alizeti kutoka tani 1.6 hadi 4 kwa kutoa mafunzo ya Kilimo bora na kutoa habari za masoko ya mazao kwa **kuanzisha kituo cha Mafunzo, Teknolojia na Habari za Kilimo** katika Kata ya Pahi. Kituo ambacho ujenzi wake umekamilika bado kuunganisha umeme ambapo zinasubiriwa nguzo za umeme. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imepanga kuweka zana, pembejeo, samani na vifaa vingine ili kituo kiweze kuanza kutoa huduma.
- Kupanua biashara ya mazao kwa **kujenga/kuanzisha masoko ya mazao katika miji mikubwa** ya Berekò, Pahi, Itaswi, Kwadelo, Kisese, Mnenia, Masange, Thawi na Busi ikiwa ni pamoja na kuimarisha utekelezaji wa mpango wa stakabadhi ghalani katika Kata za Itaswi, Bumbuta, Pahi, Kwadelo, Hondomairo na Mnenia.
- Kuongeza eneo la mashamba ya umwagiliaji kwa **kujenga miundombinu ya umwagiliaji** katika mabonde ya Kisese, Kikore, Mnenia na Kwamadebe ikiwa ni pamoja na **kuanzisha Block Farming katika Vijiji vya Kwadelo, Bomang'ombe na Ihari**
- Kushirikiana na sekta binafsi (PPP) katika kutekeleza **kilimo cha mkataba**
- **Kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji** kwa eneo la Kijiji cha Chubi lenye ekari 1,764. Halmashauri itaendelea kuwezesha uwekezaji wa ndani kwa kuviwezesha Vikundi 5 vyenye jumla ya Vijana 75 (HAPA KAZI TU) ambavyo vitalima ekari 200 za alizeti
- Kuwajengea uwezo wakulima wote juu ya **teknolojia za uhifadhi wa mazao** mbalimbali ili yaweze kuhifadhiwa kwa muda mrefu

### 3.2.1.3 Mifugo na Uvuvi

Kuongeza ubora na thamani ya mifugo kwa kuongeza uzito wa ng'ombe kutoka kg 150 hadi 250 na mbuzi kutoka kg 20 hadi 30 kwa kufanya yafuatayo: -

- Kujenga miundombinu ya soko kubwa la mifugo katika Kijiji cha Mtiryangwi.
- Kukarabati majosho 6 ambayo hayafanyi kazi katika Vijiji vya Itaswi, Salare, Salanka, Masange, Thawi na Changaa na kujenga majosho mapya 2 katika Vijiji vya Bukulu na Mtiryangwi.

- Kutoa **chanjo** ya magonjwa ya mifugo za CBPP, RVF, FMD, RABIES, LS, BQ na ANTHRAX (Ng'ombe, Mbuji, Kuku na Mbwa)
- Kuboresha maeneo ya minada kwa **kujenga miundombinu** (kujenga uzio kuzunguuka eneo la kuhifadhi wanyama, kujenga mawe ya kuchinjia Mtiryangwi, Haubi na Kwadelo, kujenga mapandishio na vyoo)
- Kuendeleza ufugaji wa samaki kutoka ufugaji wa kawaida hadi ufugaji wenye tija kwa kufanya **upembuzi yakinifu** katika mabwawa ya Haubi na Kisaki na kufanya ukarabati ikiwa ni pamoja na kuanzisha shamba la samaki katika bonde la Kisese.

#### **3.2.1.4 Ujenzi /Majengo**

Halmashauri imepanga kuongeza usimamizi katika shughuli zote za ujenzi wa majengo mbalimbali yakiwemo majengo ya ofisi, madarasa, nyumba, vyoo, maabara, hospitali, vituo vya afya, zahanati na matengenezo ya vifaa /samani kama vile madawati, vitanda, meza na viti.

#### **3.2.1.5 Ardhi**

- Kuandaa mpango kabambe wa Ardhi, kupima viwanja ( Berekwa, Masange viwanja 500 na Kisese Disa viwanja 500), na kutenga maeneo ya kipaumbele kwa shughuli mbalimbali
- Kutatua migogoro ya ardhi Vijijini kwa kufanya ziara na mikutano na wadau wote wanaohusika
- Kuondoa migogoro baina ya wakulima na wafugaji kwa kupanga matumizi bora ya ardhi katika Vijiji 10 na urasimishaji wa Ardhi kwa kutoa hati za kimila

#### **3.2.1.6 Maliasili na Utalii**

- Kuwezesha uwekezaji kwa kujenga kituo cha kutolea habari/historia za michoro ya kale ya miambani iliyochorwa miaka 30,000 iliyopita katika safu za miinuko ya Irangi iliyopo katika Kata za Mnenia, Itololo na Busi na jengo la kikoloni la Mnenia, pia kujenga nyumba za kufikia watalii/wageni, vyombo vya usafiri na kuuza bidhaa za kitamaduni
- Kuvutia uwekezaji wa ujenzi wa Chuo cha Utalii
- Kuwezesha ufugaji wa nyuki kwa kuanzisha mashamba katika msitu wa Isabe ulipo katika Kata za Mnenia, Itololo na Busi
- Kuhifadhi misitu

### **3.2.2 Huduma za Jamii**

#### **3.3.2.1 Elimu Msingi**

Katika kuboresha elimu ya msingi Halmashauri imejielekeza kutekeleza yafuatayo: -

- Kuhakikisha upungufu wa madawati hautokei kwa kusimamia ukarabati wa kila dawati litakaloharibika na kuhakikisha gharama za kujenga chumba cha darasa kinajumuisha na



madawati

- Kutenga Bajeti ya capitation, likizo, mitihani, uhamisho, matibabu na posho za walimu wakuu na maafisa Elimu wa Kata
- Kupunguza utoro wa wanafunzi kwa kuhakikisha kila shule inatoa chakula cha mchana.
- Kuandikisha watoto wa madarasa ya awali na darasa la kwanza kwa wenye umri wa kwenda shule kwa asilimia 100
- Kuwezesha vifaa vya shule kwa wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu.
- Kujenga na kukarabati nyumba za walimu, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na ofisi za walimu
- Kuendelea kuwajengea uwezo walimu wa masomo ya sayansi na hisabati

### **3.3.2.2 Elimu Sekondari**

Katika kuboresha elimu ya Sekondari Halmashauri imejielekeza kutekeleza yafuatayo: -

- Kujenga nyumba za walimu katika shule zenye upungufu mkubwa.
- Kutenga malipo ya Capitation kwa wanafunzi, likizo na uhamisho kwa walimu, matibabu na posho ya Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata
- Kuendesha mitihani kwa wanafunzi wote na kutoa chakula kwa wanafunzi wa bweni.
- Kukamilisha vyumba 12 vya Maabara na kujenga madarasa 42 ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi wanaotarajiwa kuingia kidato cha kwanza Januari 2020

### **3.3.2.3 Maji**

Katika sekta ya maji Halmashauri imejipanga kuongeza hali ya upatikanaji wa maji kutoka 32% hadi 85% ifikapo mwaka 2021 kwa kutekeleza yafuatayo: -

- Kujenga miradi mipya ya maji katika Vijiji 29
- Kufanya ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika Vijiji 17
- Kuimarisha usimamizi vijijini katika kuhifadhi vyanzo vya maji 20 kufikia 2019

### **3.3.2.4 Afya**

- Kupunguza vifo vya akina mama na watoto
- Kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba
- Kuwashirikisha akina baba katika masuala ya uzazi salama
- Kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya wa jamii (CHWs) juu ya afya ya mama na mtoto.
- Kusaidia ukamilishaji wa majengo ya vituo vya kutolea huduma za Afya

### **Kuboresha Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwa: -**

Kuongeza wanachama wa CHF kutoka 25% hadi 35% kwa kufanya yafuatayo:-

- Kufanya uhamasishaji ngazi ya jamii katika Vijiji vyote 84
- Kuboresha mfumo wa uwandikishaji kwa kuongeza vifaa na kuwafuata walengwa badala ya kuwasubiri
- Kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wanachama (kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi)

### **3.3.3 Usafi na Mazingira**

Halmashauri itajielekeza katika kufanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha na kusimamia ujenzi wa vyoo bora katika vijiji vyote vya Wilaya ya Kondo na Taasisi za Umma
- Kutoa elimu ya usafi wa mazingira katika Vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Kondo
- Kujenga vizimba vya taka katika miji midogo inayokua ya Pahi, Bereko, na Busi na Vijiji vya Mnenia na Kwadelo.

### **3.3.4 Masuala Mtambuka**

#### **Vijana na akina Mama**

- Kuwezesha Vijana na akina mama kwa kuwakopesha mitaji kwa kuwatengea asilimia 8% ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uzalishaji mali.
- Kuviunganisha vikundi vya Vijana na akina Mama na Taasisi za mafunzo ya ujasiriamali na Taasisi 31 za mikopo ili viweze kukopa na kujiendeleza
- Kuanzisha Viwanda vidogo vidogo kwa kushirikiana na Shirika la SIDO kwa ajili ya Vijana na akina Mama

## **Walemavu**

Kutokana na bajeti ya 2% ya mapato ya ndani, Halmashauri itajikita kufanya yafuatayo: -

- Kufanya utambuzi wa walemavu wapya na waliopungua katika ngazi za Kata na Vijiji kwa ajili ya kuhuisha Takwimu na kuwaelimisha wapya kujiunga katika Vikundi
- Kutoa mikopo kwa vikundi 6 vya walemavu na kutoa Elimu ya ujasiliamali
- Kuanzisha mabaraza ya walemavu katika ngazi za Kata na Wilaya
- Kuanzisha klabu 4 za walemavu

## **UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza**

- Kuendelea kuhamasisha watumishi wa Halmashauri kupima afya zao kwa kila robo mwaka kwa ajili ya kupunguza uwezekano wa watumishi kupata magongwa hayo
- Kuendelea kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wenye uhitaji katika masuala ya elimu
- Kusaidia vikundi vya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI vinavyojishughulisha na kilimo cha mbogamboga

## **Mapambano dhidi ya Rushwa**

- Kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika kubainisha mianya ya Rushwa na kuweka mikakati ya kuzuia rushwa
- Kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika kutatua migogoro ya ardhi inayosababishwa na watumishi wasio waadilifu

## **Uwazi na Uwajibikaji**

- Halmashauri itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Maadili ya Utumishi wa Umma katika kuelimisha viongozi wa ngazi zote juu ya masuala ya uwazi na uwajibikaji
- Kusimamia mipango kazi ya wakuu wa idara kuhusu ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa katika ngazi za Vijiji na Kata
- Kuendesha mafunzo kwa Viongozi wapya katika Kata, Vijiji na Vitongoji

## **Lishe**

Halmashauri imepanga kuendelea na utekelezaji wa shughuli za lishe katika sekta za Kilimo, Mifugo, Elimu na Afya kwa kufanya yafuatayo:-

- Kufanya vikao vya kujadili hali ya lishe kwa kila robo mwaka
- Kujenga makaushio ya kisasa ya mboga za majani

- Kuendelea kuongeza vikundi vya uhamasishaji lishe kutoka 20 hadi 40
- Kuendeleza bustani za mbogamboga katika vijiji 20.
- Kuendeleza bustani za mbogamboga na viazi lishe katika shule Msingi, Sekondari, Zahanati na Vituo vya Afya
- Kuendelea kutoa matone ya vitamin A kwa watoto

### **Kuongeza Mapato ya Ndani na kudhibiti Matumizi ya Fedha**

Ili kuwa na takwimu sahihi za mapato ya ndani, orodha ya walipa kodi, ukusanyaji wa uhakika na kupunguza uwezekano wa upotevu wa fedha, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:

-

- Kuendelea kutumia mifumo ya kielektronik katika makusanyo ya fedha (kodi ya majengo, ushuru wa mazao, ushuru wa minada, ushuru wa soko) kwa kushirikiana na Mradi wa LIC (Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji) ambapo mashine za kielektronik (POS) zitaongezwa kutoka 22 hadi 65.
- Kujenga stendi ya kisasa ya mabasi katika mji mdogo wa Bereko ambayo itakuwa pembezoni mwa Barabara ya Dodoma – Kondoa – Arusha
- Kupima na kuuza viwanja katika miji midogo ya Bereko, Pahi, Bukulu, Haubi, Busi, Kwadelo, Mnenia, Alagwa na Masange. Ambapo jumla ya viwanja 1,200 vitapimwa na kuuzwa.
- Kujenga mazingira mazuri yenye kuvutia biashara katika maeneo mbalimbali ya biashara (minada na masoko)
- Kufanya mapitio ya sheria ndogo za Halmashauri ili kurekebisha viwango vya tozo mbalimbali
- Kuwezesha upatikanaji wa gari la mapato

### **Miradi ya Kimkakati**

#### **Mhe. Mwenyekiti;**

Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imeanza kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa itakayojengwa pembezoni mwa Barabara ya Arusha – Kondoa – Dodoma. Andiko la Mradi litawasilishwa mwezi Aprili 2018.

## Maombi Maalumu

### Mhe. Mwenyekiti;

Halmashauri inawasilisha maombi maalum mawili (2) kama ifuatavyo;-


1. Halmashauri inawasilisha ombi maalum la **Tsh. 2,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali kama awamu ya kwanza. Kondoza Vijijini inajumla ya Vituo vya Afya 6 na Zahanati 34 ambazo zote hazina Hospitali ya referal na hivyo kutegemea Hospitali ya Mji Kondoza ambayo imeelemewe kutokana na kuhudumia watu zaidi ya 700,000 kutoka Wilaya ya Chemba, Kondoza Mji, Kondoza Vijijini na Wilaya za jirani.
2. Halmashauri itawasilisha ombi maalum la **Tsh. 1,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika bonde la Kisese. Eneo litakalomwagiliwa ni ekari 5,000. Mradi huu utatarajiwa kuingiza faida ya Tshs. 2,957,600.00 kwa ekari 1 kwa mwaka sawa na faida ya Tshs. 14,788,000,000.00 kwa ekari 5,000 kwa mwaka. Mradi utatoa fursa ya ajira kwa Vijana zaidi ya 10,000.

### Mhe. Mwenyekiti;

Katika kutekeleza vipaumbele hivi, Halmashauri inategemea kukusanya fedha **Tshs. 30,610,933,906.00** kutoka katika vyanzo vifuatavyo:-

Ruzuku ya Matumizi Mengineyo	2,188,640,848.00
Ruzuku ya Mishahara	15,373,360,600.00
Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	12,482,479,362.00
Mapato ya Ndani	1,097,253,064.00

Kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha mapendekezo haya ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019,



(Mwl. Falesy Mohamed Kibassa)

**Mkurugenzi Mtendaji (W)**

**KONDOA**